**JINA........................................................................ NAMBARI YA USAJILI ..............................**

**SHULE................................................................... DARASA/MKONDO.....................................**

**TAREHE .............................................................. SAHIHI ..........................................................**

MTIHANI WA KISWAHILI
KARATASI MSETO
KIDATO CHA PILI
MUDA:SAA2 ½

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| ISIMUJAMII | 10 | |
| FASIHI SIMULIZI | 15 | |
| **Jumla** | **80** | |

**MAAGIZO**

- Andika **jina lak**o, **nambari yako** ya usajili, **jina la shule** na **darasa/mkondo** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia **sahihi yako** kisha uandike **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapojuu.
- Jibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cia maswali.
- Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili
- Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

***Karatasi hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo***

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma makalayafuatayo kisha ujibu maswali:***

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake waliosihi mapote mawili yaliyopita ; wanawake makamu ya nyanyake na mamake - kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto, na daima dawamu kuwa ***"mwandani wa jikoni"*** akawapikia watoto na bwanake chakula ; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani, kuchanja kuni,, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. ***Akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake.***

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo yake ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa ***hateswi akafyata ulimi***. Anapohiniwa yeye hupigania haki kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katikajamii alipotengwa na wanaumme wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati.
Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha ***ukutani***.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katikajambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani yale ya kale, lakini wapi! Analazimika kukubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya ***aushi***.

(a) Msemo ***'mwandani wa jikoni'*** unadhihirisha bali gani ya mwanamke katikajamii? (alama 2)

________________________________________

________________________________________

(b) Jamii imefanya mwanamke kuwa hayawani wa mizigo. Fafanua (alama 2)

________________________________________

________________________________________

(c) Eleza maana ya **'akanyagapo mumepapo huutia wayo wake'** (alama 2)

________________________________________

________________________________________

(d) Mlinganishe mwanamke wa kiasili na wa kisasa katika maswala ya ndoa na elimu (alama 4)

(e) Mwanamume wa kisasa anamwonaj e mwanamke wa kisasa? (alama 2)

(g) Eleza maana ya:

(i) Akafyata ulimu (alama 1)

(ii) Ukutani (alama 1)

(iii) Taasubi za kiume (alama 1)

**2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 15)**

1. Taja sauti zozote mbili zinazotamkiwa kwenye midomo. (alama 2)

2. Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi; nilimchapa. (alama 2)

3. Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hlii;
Alimpigia mpira. (alama 2)

4. Pambanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo cha mstari.

i) Mtoto wake amepotea. (alama 3)

5. Yakinisha sentensi ifuatayo:
Chakula chake hakiliki. (alama 2)

6. Unganisha kwa kiunganishi mwafaka. (alama 2)

i) Siendi ii) Sichezi

7. Tia mkazo/shadda katika neno hili ili kuleta maana mbili tofauti. (alama 2)
Walakini

8. Akifisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti kuonyesha umuhimu wa kiimbo. (alama 3)
Ameenda sokoni

9. Tambua ngeli za nomino hizi (alama 2)

i) Mitume ______________________________

ii) Kamusi ______________________________

10. Andika kwa hail wastani wingi (alama 2)
Majibwa haya yalibweka yakayahofisha majitu yale.

11. Taja ama mbili za mofimu kwa kutoa mfano mmoja mmoja kwa kila ama. (alama 2)

12. Akifisha (alama 3)
Salaale haya ndiyo mambo aliyotuitia mmoja wao aliuliza.

13. Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi **'-ingi'** katika ngeli ya KI-VI umoja. (alama 2)

14. Eleza maana ya misemo ifuatayo, (alama 2)

i) Paka mafuta kwenya mgongo wa chupa.

ii) Ambulia patupu.

15. Tunga sentensi sahihi ukitumia visawe vya maneno yafuatayo. (alama 2)
i) Tabibu

ii) Mwalimu

16. Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti kati ya maneno haya: (alama 2)
Chakura na chakula

17. Tambua na kuainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo (alama 4)
Mtoto ameenda kusoma shuleni

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
a) Eleza maana ya sajili (alama 2)

b) Fafanua sifa nne za sajili ya hotelini (alama 8)

**FASIHI SIMULIZI**

1. Eleza maana ya nyimbo katika fasihi simuli. (alama 2)

2. Taja sifa zozote tatu za nyimbo (alama 3)

3. Fafanua aina zozote tatu za nyimbo (alama 6)

4. Eleza dhima nne za nyimbo katika jamii. (alama 4)